

Ibada Ambayo Mungu Anakubali (Sehemu ya 2)

Inategemea sura ya 15 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kinachopatikana kwenye jw.org/sw.

LENGO: Chunguza mambo unayoamini na sababu za kuamini mambo hayo, chunguza kile ambacho Biblia inafundisha, na uone jinsi unavyoweza kuwaeleza wengine mambo unayoamini.



JE, INATOSHA TU KUMWAMINI MUNGU?

1 CHUNGUZA MAMBO UNAYOAMINI

Kwa nini huenda baadhi ya watu wakajibu ndiyo?

Kwa nini huenda baadhi ya watu wakajibu hapana?

Wewe unaamini nini?

Kwa nini unaamini hivyo?

Tunapaswa kumwabudu Mungu kwa njia anayoikubali.

(Ona sura ya 15 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 15-18.)

Soma Yakobo 2:19.

Mstari huu unaonyeshaje kwamba tunahitaji kufanya mambo mengi zaidi ya kumwamini Mungu tu?

Soma 2 Wakorintho 6:17.

Ikiwa tunataka Mungu 'atukaribishe ndani,' au atukubali, tunapaswa kufanya nini kuhusiana na ibada ambayo haikubali?



Kumtumikia Mungu pamoja na watu wake kunatuletea baraka nyingi

Tunafaidika sana tunapomtumikia Yehova pamoja na watu wake.

(Ona sura ya 15 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 19-20.)

Soma Marko 10:28-30.

Yesu alisema wafuasi wake watapata baraka gani sasa na wakati ujao?

Soma 2 Petro 3:9, 13.

Kwa nini ni jambo la hekima kufanya yote tuwezayo ili kumwabudu Mungu kwa njia anayoikubali?

Umenufaikaje kwa kumwabudu Mungu pamoja na watu wake?

3

ELEZA MAMBO UNAYOAMINI

MTU AKISEMA . . .

Jambo la maana ni kumwamini Mungu tu.

UNAWEZA KUSEMA HIVI . . .

Ni kweli kuamini kwamba Mungu yupo ni jambo la maana. Lakini nimetambua kwamba tunahitaji kufanya mengi zaidi ya kuamini tu kwa sababu . . .

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje kuelewa andiko hilo?

MTU AKISEMA . . .

Huhitaji kuwa mfuasi wa dini fulani ili umpendeze Mungu.

UNAWEZA KUMJIBU HIVI . . .

Huenda watu wengi wakakubaliana na maoni hayo. Lakini ninaamini jambo tofauti kwa sababu . . .

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje kuelewa andiko hilo?